## BODI YA UTAWALA CHUO CHA UFUNDI ARUSHA YAPONGEZA UJENZI MRADI WA KUFUA UMEME KIKULETWA

- **UJENZI WAFIKIA ASILIMIA 77**



*Mwenyekiti wa Bodi ya Utawala ya Chuo cha Ufundi Arusha (Katikati)* ***Dkt. Noel Eusebius Mbonde*** *akiwa kwenye picha ya Pamoja na Wajumbe wa Bodi wa Chuo hicho walipotembelea eneo la ujenzi wa mradi wa kufua umeme kampasi ya Kikuletwa*

Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) kimepongezwa kufuatia usimamizi mzuri wa ujenzi wa mtambo wa kufua umeme unaojengwa katika Kampasi ya Kikuletwa iliyopo wilaya ya Hai mkoa wa Kilimanjaro utakaotumika kuzalisha umeme na kutoa mafunzo kwa vitendo.

Akizungumza baada ya kutembelea mradi huo Mwenyekiti wa Bodi ya Utawala ya Chuo cha Ufundi Arusha Dkt. Noel Mbonde amepongeza uongozi wa Chuo kwa usimamizi mzuri katika hatua za ujenzi wa mtambo huo.

“Nawapongeza Bodi ya Chuo ambao wamekua wakifanya kazi bega kwa bega na uongozi wa Chuo kuhakikisha kwamba mradi huu unaendelea kama ulivyopangwa, inabidi tuendelee na huu utaratibu wa kutembelea miradi, sio huu tu bali miradi yote ya Chuo cha Ufundi Arusha” alisema Dkt. Mbonde.

Vilevile Dkt. Mbonde amemshukuru rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha za ujenzi wa kituo hicho.

"Nichukue fursa hii kumshukuru rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki, na pia shukrani nyingi ziwaendee viongozi wetu wa Wizara kwa kusimamia kwa makini sana maendeleo ya ujenzi wa kituo hiki" alieleza Dkt. Mbonde.

Aidha Dkt. Mbode alifafanua kwamba lengo la mradi huo ni kusaidia kuzalisha umeme Kwenda kwenye gridi ya taifa na pia utatumika kama kituo cha mafunzo ya uzalishalishaji wa umeme kwa wanafunzi watakaosoma fani za mafunzo ya umeme.

Mtambo huo wa kufua umeme unajengwa kupitia mradi wa Afrika Mashariki wa kujenga ujuzi kwa mlingano na uingiliano wa Kikanda (EASTRIP) kupitia fedha za Benki ya Dunia ambapo mpaka sasa umefikia 77% kwa awamu ya kwanza na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Oktoba.














